# U D A N G A N Y I F U

*2Yohana 1:7:11*

*‘‘kwa maana wadanganyifu wengi wametokea duniani. Wasiokiri ya kuwa Yesu Kristo yuaja katika mwili. Huyo ndiye mdanganyifu na mpinga Kristo.Jiangalieni nafsi zenu msiyapoteze mliyo yatenda, bali mpokee thawabu timilifu.Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu.Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia’’.*

Acha tusikie ambacho, Nabii wa Mungu William Branham amesema juu yake:

Hebu chukua yoyote ya mabatizo hayo ya uongo, fulani na fulani za uongo, sijali linavyo sikika kuwa halisi. Jinsi wanavyo jaribu kuiga, ni uongo kama ni kinyume cha Neno la Mungu la wakati huu. Hiyo ni kweli hasa. Unasema ‘‘vema, tulifanya jambo hili na tunafanya jambo hili, na kanisa letu ni namna hii, na namna ile.Sijali nini.Kama ni kinyume cha Neno lililoandikwa la wakati huu ni uongo. Mungu hatakuwa na uhusiano wowote nalo, haidhuru ni aminifu namna gani. Ni la kielimu jinsi gani, ni la akili jinsi gani, linasikika ni kweli jinsi gani, laonekana la hekima jinsi gani.Iwapo ni kinyume cha Neno la wakati huu…….

Haijalishi ni jinsi gani muhubiri anaweza kuhubiri kwa nguvu, vema jinsi angeweza kufanya lionekane, kama ni kinyume cha Neno.Liachilie mbali nawe. Kaa mbali, msafi. Ni Neno tuu ndio mpango wa Mungu, Ufunuo mkamilifu wa kile alicho kuwa, kile alicho, na kile atakacho kuwa ni mwendelezo wa Ufunuo wa Yesu Kristo na Ufunuo wa Yesu Kristo ni Biblia.Chochote kilicho funuliwa kinyume na Yeye/kusema vile angelifanya, vile alivyo…..jamani, hilo lilikuwa katika siku zilizopita usiamini hilo/ ingelipaswa kuwa Yesu yule yule, unaona na hiyo ni Neno.

Leo, wamechanganyikiwa sana juu ya ushahidi wa Roho Mtakatifu, na kadhalika.Shetani anaweza kuigiza kipawa chochote alichonacho Mungu, bali hawezi kuleta hilo Neno, Neno kwa Neno. Hapo ndipo aliposhindwa katika bustani ya Edeni hapo ndipo ameshindwa daima hapo ndipo ile kanda ya watiwa mafuta wa uongo ama watiwa mafuta….wao wanaweza kutiwa mafuta na Roho, wa-nene kwa lugha ,wacheze dansi, wapaze sauti, wahubiri injili, na wangali ibilisi. Ni kule ndani. Sasa kumbuka, Yesu alisema. ‘‘Wote alionipa Baba watanijia mimi.Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba yangu kwanza’’(Yoh. 6:37:44).

Sasa, jambo lile lile ni hili: Iwapo wewe ni Mwana wa Mungu, na kama mimi ni Mwana wa Mungu, au binti wa Mungu, tulikuwa katika Mungu hapo mwanzo.Na wakati Yesu alipofanyika ukamilifu wa Neno ndipo tulipokuwa ndani Yake jinsi ya chembechembe hai.Hapo Yeye aliposulubiwa sisi tulisulubiwa katika mwili wake(Rum 6:6,Gal,2:20). Hapo alipofufuka katika wafu, tulifufuka pamoja naye.Na sasa kwa kuwa tumetambua jambo hilo sasa tumeketi pamoja Naye katika ulimwengu wa Roho katika Yesu Kristo unaona? Kwa kuwa kama sisi ni watoto wa Mungu, wa kike na wa kiume basi sisi ni sehemu ya Mungu.Tulikuwa tuna uzima wa milele naye Mungu ndiye uzima wa milele uliopo.Basi tulikuwa ndani yake tangu mwanzo.Na wakati Yesu alipofanyika hilo Neno lote, basi tulikuwa sehemu yake wakati huo. Amina.Haya basi kitu hicho kinapo kuwa humo ndani hakuna ibilisi, hakuna mamlaka, hakuna kitu kinachoweza kukitikisa. Hicho ndicho nguzo ya kushikiza ya Nafsi.

Unaweza kupakwa mafuta hapa nje katika Roho, na upate shauku, na kufanya haya mambo mengine yote, bali inapofikia nguzo hii ya kushikiza kwa hilo Neno, hutaondoka pale kamwe. Itashikilia moja kwa moja kwa uthabiti na uaminifu, kwenye Neno hilo. Jinsi inavyoweza, nje ya jambo hilo haidhuru utafanya nini, ungali umepotea. Huo wakati wa kanisa la Laodikia, ‘”Uchi, kipofu, wenye mashaka; wala hata haujui. Unaona,Roho Mtakatifu huyu anaweza kumshukia mtu katika Roho yake bali Nafsi yake ndio chembe cha Neno. Unaona? Sijali jinsi unaweza kuhubiri kiasi gani ni vizuri, jinsi gani unatenda jambo, hili na kiasi gani unavyopenda…….huo ni mmoja wapo wa milango ya Roho.huwezi kupenda kwa mwili wako, unapenda kwa Roho yako.Huo ni mmoja wapo wa ile milango ya Roho.Nawe unaweza kupenda na hata umpende Mungu na hata hivyo usiwe sawa. Unaweza kutoa pepo na kuhubiri na kufanya mambo hayo; hata hivyo usiwe sahihi.Yesu alisema hivyo, alisema wengi wangekuja kwenye siku hiyo. Hilo, Neno latosha (Mathayo 7:21-23)

Unasema, vema, jamani, mimi ni mpentekoste; kama hauko sambamba na hili Neno, kuna jambo fulani si sawa. Unaona? Baadaye unaona, Baba yako halisi si Mungu, kwa sababu hilo kwa uhalisi lilianzia katika Nafsi yako kabla hata hakuja kuwepo na Roho, Nafsi yako ili kuwepo. Nafsi hiyo haikutoka kwa Mungu, kwa hiyo haikuwa chembe chembe ya Mungu tangu mwanzo.Umedanganywa. Wewe ni gugu lililo

pandikizwa na ukizaa historia ya Ulimwengu wa magugu, ukija na kutenda kama ulimwengu. Ukiupenda ulimwengu, ni kwa sababu upendo wa Mungu hauko ndani yako.

Mjumbe Martin Alisema, Shetani alimtokea wakati mmoja, amevaa taji kubwa ya Dhahabu, nyota tatu au nne ndani yake kama namna hiyo, akimetameta na yu mzuri, mtanashati, amechana vizuri na msafi, amevalia vazi zuri, na viatu vyake miguuni mwake vilikuwa vya dhahabu, akitoka nje na kusema, Martini, je unanijua mimi?

Sasa,watu ambao hawaoni maono,unaweza usielewe, bali vitu vinavyoweza kukujia katika roho tofauti na jinsi vinavyodanganya. Biblia inasema wangelidanganya yamkini hata walio wateule kama ingewezekana.

(Mathayo 24:24). Unaona? Wateule, hao ndio ambao wamechaguliwa toka awali na kuzaliwa kwa kusudi hilo.Kwa hiyo alimjia huyo aliyeteuliwa yeye alisema‘‘Martini”, unanitambua? Mimi ni Kristo je unanitambua mimi? Martini alisita: Ilionekana la kigeni. Kasubiri dakika moja, Na shetani akasema tena, “ Je hunioni? Mimi ni Kristo. Je unanitambua? Akamwambia namna hiyo mara tatu au nne. Kristo akasema au Martini akasema, “ shetani ninakujua, Bwana wangu hajavikwa taji bado, bali watakatifu wake watamvika taji’’. Neno lipo pale.

Kwa hiyo ati kwa sababu tu, tunaweza kuchangamka, haimaanishi kwamba tumeokolewa. Kwa sababu tunaenda kanisani haimaanishi kwamba tumeokolewa. Usiziamini hizo roho zinazo shawishi. Roho halisi wa Mungu Neno halisi la Mungu ni kweli ya Mungu ambayo ni mbegu ya Mungu itamzaa Mungu maishani mwako uwe mcha Mungu, mtauwa Mtakatifu. Miongoni mwa watu wengi tunaona mahali ambapo mchangamko na kadhalika kunakuwako na kupayuka payuka na kusengenyana na kila aina ya mambo yasiyo ya kiungu ndugu, hiyo ni asidi ya sumu kanisani; Ni nguvu ya kipepo.Roho za wanaume na wanawake wanazo shirikiana mmoja kwa mwingine na kujaribu kusukuma mbali kusema, jambo hili sio sawa na lile si sawa kama ukilifuatilia mara tisa kwa kumi ni mtu huyo huyo anaye chochea watu ambaye hayuko sawa. Amina. Mungu anachukia mafarakano kati ya ndugu iweni wenye uchaji, iweni watakatifu mpendeni Mungu shikamaneni naye na mradi unajua maisha yako yanaambatana na Biblia ukiwa na moyo safi wa mawazo, upendo kwa ndugu yako, ukijaribu vizuri kuujenga ufalme wa Mungu na kufanya mambo hayo ukivaa inavyopaswa ukiishi sawa ukizungumza sawa ukienda sehemu zinazofaa ndipo unaweza kuwa na Misisi mko yote unayotaka kuwa nayo na kila mtu ataamini jambo hilo**.**

Yesu alisema ninyi ni chumvi ya dunia lakini chumvi ikipoteza ladha yake haifai kabisa ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu (Mathayo 5:31) kama wewe ni chumvi pekee,hilo siyo zuri. Lakini kama wewe una ladha ndani yako wewe uwe umekolea chumvi wao wataona kiu lo! Jamani roho zinazoshawishi zikitoka kwenda, pepo zilizojificha.

Angalia tuko katika siku za mwisho tuko katika wakati wa mwisho ulimwengu uko karibu, tayari kufikia upeo wake wa hatari kama jipu linalo uma sana mahali fulani litakapopasuka moja ya siku hizi na kiini chake kitoke ndani yake.Umekuwa mchafu hakuna dawa inayoweza kukiponya. Wao wamekataa dawa inayowezakuponya. Wao wamekataa ile chango. Wamekataa matibabu ukichukuwa jipu linalo vimba pale na kama hudungwi penicillin au kitu cha kuliondolea mbali au chochote kile litaendelea kuvimba mpaka litapasuka.Hivyo ndivyo ulimwengu ulivyofanya ulianza si muda mrefu uliopita kuachilia. Walienda kando juu ya wazo kubwa pepo wa uongo wakaja na kuwaambia watu hivi na vile na vinginevyo tumevunjika katika madhehebu mia tisa na kitu. Kila mmoja akiwa na maoni tofauti wanasema tunaamini jambo hilo.Hivi tu hivyo.Ndivyo tunavyo amini. Hawawezi kumruhusu Roho Mtakatifu aingie.Hawawezi kuwa na njia sahihi. Mungu akipata kundi la watu ambao waliweza kushangilia Basi kila mtu ilimbidi kushangilia. Wakawapata wengine ambao wangenena kwa lugha wakafanya yote mpaka ikawa kitu gani, kitu kilicho pagawa na roho zinazoshawishi kabisa zikawashawishi watu kufanya na na kuchangamka huku wakati hakuna Mungu ndani ya jambo hilo hata kidogo ndipo wanatoka na kuishi maisha yoyote wanayopenda kuishi halafu wanaita hicho ni Ukristo (1Tim, 4: 1,-5).

Unajua, hiyo imekuwa ni shida. Ninazungumza na Wakristo na Wahuduma. Na nataka kuwa mwaminifu juu ya mambo haya.Na hapo ndipo hata wahudumu wengi wanafanya makosa.Tumesikia mara nyingi sasa juu ya Wahudumu, Matendo wanayoyafanya na mambo wanayofanya. Wengi wao labda wanafanya mambo wasiopaswa kufanya nafikiri mara nyingi sana, wao ni watu wazuri Wakristo wa kushangaza sana ambao wamekuwa wakitumiwa na Bwana. Na halafu mwishowe wamepata Ufalme mdogo uliojengwa ukiwazunguka, ama ushawishi sana, watu wengi wanahudhuria mikutano yao, mpaka wanakuwa wasiojali, na wanapata namna ya kuinuliwa juu, watu wana watukuza wao na kuwaunga mkono, na hakika tusingepaswa kufanya hivyo. Sisi, kumbuka,sisi wote tu…….

Hakuna watu walio wakuu miongoni mwetu.Kwanini, sisi sote ni watoto tu wa Mungu.Mnaona? Ikiwa Mungu amemfanya mmoja wetu kitu kimoja na mwingine kingine kwanini, ameniumba mimi nikiwa na kidole na macho, na kadhalika,vema, hatuna budi kufurahiana, na basi si kujiona

umkuu.Kwa sababu sisi sote tumeunganishwa katika Mungu mmoja na sisi sote tumetolewa katika mti mmoja.

Haidhuru umekuwa,Mkristo kwa muda mrefu kiasi gani na ungali una hizo roho za kale zinazo zungumza nawe zinakufanya ushikwe na hamaki zinakufanya kumsengenya mtu fulani, wakati mtu fulani anapokuja na kuanza kumsengenya mtu mwingine unaungana moja kwa moja nao lo! Una wararua tu hilo ni kosa ndugu usifanye hivyo hilo hatimaye litakuzuia kuingia katika ile Nchi ya ahadi na kama una mambo madogo ya miaka mingi ambayo hupaswi kuwa nayo kama upendo wa Mungu kweli haumo moyoni mwako, si uwe bibi na mwanaume kweli kweli uje hapa na kusema. Mungu nitatupa papa hapa asubuhi ya leo papa hapa nitaondoka. si uje?(1Tim, 6:3-5).

Hivyo ndivyo shida ya watu leo.Hawawezi kumngoja Roho Mtakatifu halisi kulitoa kanisa katika mahali pake.Inawapasa watengeneze kitu fulani.Walifanyie kazi jambo fulani:Ishara ya kwanza kunena kwa lugha, kupata washiriki zaidi kanisani,mambo haya yote ya kipuuzi. Badala ya kumsubiri Bwana kwa madhihirisho halisi ya kufufuka kwa Kristo akijifanya Yeye Mwenyewe ajulikane miongoni mwa watu hawawezi kusubiri. Naam,haijalishi uwapi, kama haujazaliwa kwa Roho wa Mungu na kupokea Roho Mtakatifu…wa Mungu na kupokea Roho mtakatifu…..na sababu…Kama hauamini Neno lote la Mungu,haujapokea Roho Mtakatifu bado hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa.Roho Mtakatifu unapo isikia kweli na Roho Mtakatifu hakuongozi kwenye hiyo, ndipo hapo pana Roho mwingine ndani pale akikuweka mbali na kitu hicho.Hivyo roho uliye mpata ndani yako siyo Roho Mtakatifu(Yohana 16:13) sasa,tunagundua kama Yanne na Yambre walisimama kinyume na Musa, jinsi ambayo mambo haya yangelikuwa katika siku za mwisho. Sasa, na nukuu ya mwisho tuliyo kuwa nayo, ilikuwa Mungu ambaye aliumba kila mbegu izae kwa jinsi yake, hiyo ni yake (Mwanzo 1:11:12; 26-27). Unaona? Kisha alipoumba mtu wake katika mfano wake, alikuwa ni mbegu ya Neno Lake. Na Yesu alipofanyika mwili, Yeye alikuwa ni mwili wa Neno la Mungu (Yohana 1:14).Na wakati tunapolipokea Neno la Mungu ndipo tunakuwa Neno la Mungu katika miili yetu, unaona? Kanisa halina budi kuwa katika hali hiyo.

Yeye alikuwa Neno, na yule bibi arusi atapaswa kuwa Neno, Neno lililo ongezwa kwa Neno lililo ongezwa kwa Neno, kuhesabiwa haki kwa Luther; kutakaswa kwa Wesley.Ubatizo wa Kipentekosti na Roho Mtakatifu, kurejeshwa kwa vipawa.Na mengineyo yote yaliyo ambatana nayo. Yapasa liwe Neno juu ya Neno, Mbegu juu ya Mbegu, maisha juu ya maisha kuleta utimilifu mkamilifu wa yule Bibi arusi wa Bwana Yesu Kristo. Sasa kumbuka ulikuwa na tabia zile za sasa jambo ni kuwa baada ya kupata mambo hayo kuwa Kristo anakuja kwa ajili ya Bibi arusi wake sasa tunaingiaje katika Bibi arusi? Sasa hilo ndilo swali wengi husema jiunge na makutano yetu mmoja wao ataka ubatizo wa aina fulani mmoja ataka kufanya hili au kile mmoja alisema lazima unene kwa lugha au hujampata, huyu asema lazima ucheze katika Roho mwingine alisema haikupasi kunena kwa lugha.Huyu asema lazima upige kelele.Huyu ana msisimko yote ni mazuri lakini bado yote si sahihi mwanaume au mwanamke, aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu angewezaje kukana Neno la Mungu, Mungu mwenyewe alifafanua na kusema.Hii ndiyo niliahidi nayo ndio hii, akionyesha tu dhahiri kama iwezekanavyo naam lazima waione kwa vyovyote vile mwaona? Kristo angekanaje Neno lake mwenyewe? Ikiwa Kristo yu ndani yako Yeye hawezi kukana Neno lake mwenyewe.

Na sasa, kutakuwepo na watiwa mafuta wa uongo katika siku za mwisho,Si Yesu wa uongo; wasingelisema namna hiyo, bali watiwa mafuta wa uongo hao ni wapinga Kristo.Wametiwa mafuta kwa Roho kutenda ishara na maajabu ambayo Kristo alifanya,bali hawataungana na Neno lake.Mnaona? Wengi watanijia siku ile na kusema, ‘‘Bwana, tulibashiri na kutoa pepo kwa jina lako,”Yeye atasema‘‘ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu, kamwe hata sikuwajua.” Nilikuwa Mpentekoste,Bwana,utukufu kwa Mungu nilipiga makelele; nilinena kwa lugha; niliweka mikono yangu juu ya wagonjwa na kuwaponya, kutoa mapepo.Ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu, kamwe sikuwajua” unaona ninacho maanisha(Mathayo 7:21-23). Loo, watoto wadogo,leo mnasikia uhitaji wa wa hivyo vitamini usiku huu, kwamba jambo fulani…..Kuna mwili unaongojea huko ng’ambo, kuna mwili unaosuburi kupokelewa.Watu, msidanganywe. Msidanganywe. Ibilisi ni mdanganyifu. Hata vazi la harusi, lazima ulivae.Lazima iwe ( Mathayo 22:1-14).

Hawa alikuwa na Neno.Shetani yu kinyume na Neno na tazama. Mara tisini na tisa na tisini-tisa mia yake, shetani alikubali kuwa ni sahihi.Karibu sana, Biblia ilisema, katika siku za mwisho ingeliwadanganya yamkini hata walio wateule (Mathayo 24:24). Ona jinsi inavyoingia? Ona vile ilivyokuwa? Ona inavyomalizwa? Njia ile ile: Muunganiko wa kutoamini Neno lote la Mungu.Umelipata hilo? Hiyo ndiyo inayoleta kifo ni kuunganika kutokuamini na Neno.Kutokuamini;sehemu ndogo tu ya hiyo, kidogo tu, nukta tu, mia moja na pasenti moja.Bali ni lazima iwe asilimia mia moja hiyo tu.

Nabii akizungumza juu ya Daudi akirejesha sanduku tazama, kwa kufanya hivi, alisababisha kifo cha mtu mwaminifu, akiweka mikono yake juu ya sanduku la agano ambapo asingelipaswa kufanya hivyo.Mkuu, mtu

mwaminifu wazia mpakwa mafuta na kila kitu kilikuwa sawa, bali sanduku lilikuwa katika njia isiyo sahihi ‘‘NG’OMBE” Biblia ilisema, ‘‘walikungwaa” si Walawi.

(2 Sam. 6. 11).Ng’ombe walikungwaa na gari lilikuwa likianguka; na mtu mwaminifu, moyo wake ulijawa na upendo, akiweka mikono juu ya sanduku kushikilia, na alipigwa akafa, kwa sababu hakuna mtu ambaye angeliweza kushika ila Walawi. Unaona Mungu jinsi anavyolitunza Neno lake, anavyotunza amri zake? Njia zake anavyotunza amri zake? Uzia alipigwa kwa ukoma (2Nyakati 26:16-21).Yuko pale Daudi,alisababisha kifo cha mtu kabisa,na uharibifu mkuu; akiwa amepakwa mafuta na Roho, wote hao,Lakini nje ya njia za Mungu. Hiyo ni kweli yeye alikufa.Oh,ilimwogopesha Daudi hata kifo; alipaita jina hapo mahali, kama ndugu Jack alivyo soma.Alimtia alama pale.Ni mara ngapi madhehebu yametenda jambo lile lile kwa waaminio waaminifu.Kanisa Katholic,Wamethodisti, Wabaptisti, Kanisa la Kristo, hata Wapentekosti, wamesababisha vifo vingi vya kiroho kwa jambo lile lile. Inapokuja, na mambo haya,wamegundua……na hawawezi kuendelea zaidi, kwa sababu hivyo ndivyo madhehebu yao yanavyo amini. Tazama leo, Mikutano, Mikubwa, jambo lile lile Hawatendi jambo lolote bali wanafanya zaidi wana wa kuzimu waliofungwa mara dufu,wabaya zaidi kuliko walivyokuwa katika sehemu ya kwanza.Wakiwafanya wagumu halisi kuja katika ukweli.Wakiwa na moja ya hii mikutano mikuu ya uamsho,na wote wao wakiingia wakaendelea kwa kitambo kidogo tu,na kutoka tena na wanaanza dhambi hizi zote tena.Wakisikia ufufuo mwingine,wanasema,”Nilikuwa na mambo mengi sana niliujaribu:hakuna lolote nililopata.”Unaona? Hawajui njia.Mungu anayozungumzia…………..

Ulimwengu siku hizi, tunaona ya kwamba kuna watu,(Biblia inabashiri jambo hilo)tabaka tatu za watu.Moja ni ya baridi ngumu; ya kawaida isiyojali nao wanaendelea tu,kwenye loji, wao huenda kanisani,wanazungumza kidogo tu juu ya hiki, kile na juu ya Bwana, na kadhalika,wanarudi,Bali hawana ujuzi halisi wa kuzaliwa mara ya pili.Loo,wengine wao wanadai jambo hilo,lakini maisha yao yanadhihirisha kuwa hawana hilo unaona? Hilo ni kwa upande mmoja, kule mbali sana. Na sasahapo chini upande wa pili, washupavu wa dini…na kanisa halisi la kweli…Yesu alisema jambo hilo, ‘‘wangefanana sana, ingewapoteza walio wateule”sasa,watu wengi’;mara waonapo ushupavu wa dini umechanganyikana na walio kweli, ‘‘A.-ha” wao wanasema, ‘‘hakuna lolote kwake” wanaendelea mnaona, hilo ni jambo lile lile Mafarisayo walilofanya.Shetani, hajapumbaza kwa kujaribu kupotosha hilo.Yeye anajaribu kupotosha kweli hii. Na huyu mshupavu wa dini hapo anajaribu kuigiza kweli ile.Unaona?**Hapo ndipo mstari wako wa hatari ulipo,papo hapo.Sasa, inatupasa kudumu kiroho kusoma Neno,na jambo lolote likizuka nje, kinyume cha Neno,basi litupilie mbali**.

Shetani atakupa kila aina ya ahadi hizi zote,bali hana chochote cha kukupa kwa sababu hana chochote.Yeye hana wokovu shetani ni nini? Kitu chochote kilicho kinyume na Neno.Yeye hana wokovu.Yeye hana nuru.Ufalme wake ni wa giza”, mwisho wake ni kifo,giza na kifo ni ufalme wa shetani. Ndugu branham, rudia hayo tena ufalme wa shetani ni upi? chochote kinacho pingana na Neno la Mungu.

Angalia,Lusifa anaingia,Mwerevu,kama alivyofanya wakati ule,na kwa majaribu na ahadi za uongo,za nguvu nje, mbali na Neno la Mungu.Alifanya hilohilo pale Nikea, Rumi, anafanya hilo hilo leo kwenye muungano wa Makanisa ulimwenguni.

‘‘Acha sisi sote tuungane pamoja” Papa anasema,” nawataka ndugu wote wa muungano wa makanisa ulimwenguni kuungana na mimi sisi ni mmoja”Hiyo ni kweli, katika vikundi ni wamoja. Lakini hilo halihusiani na Bibi arusi; si lolote,ndugu.Kamwe hutamwosha katika kitu kama hicho.

Loo! Unasema, ‘‘lakini hebu ngoja kidogo;sisi tunahubiri Neno”Angalia nyuma hapa kwenye somo langu,usiku wa leo.Shetani ndiye ambaye alimhubiri hawa Neno kwanza. ‘‘Mungu alisema (Mwanzo 3:1-7) Mnaona? **Ni kule kupotosha sehemu hiyo ya andiko ambalo linahusu wakati huo.**Atakuachilia ujue yote yale Musa aliyotenda yaliyotenda yalikuwa sawa kabisa. Lakini unapochukua ahadi hizo ambazo wamenena kwa ajili ya siku hii; basi hizo zilihusika na wakati mwingine.Hivyo ndivyo tu apaswavyo kufanya, ni kuwafanya watu kuliamini hilo.Namna hiyo, na hilo tu.Kwani hawawezi kuondoa Neno moja kwalo,wala kuongeza Neno lakini hilo ndilo afanyalo. Siku zote kumekuwepo na mapacha.Na hiyo ndiyo sababu ……**usilisahau hili,kundi dogo.Kanisa katika siku za mwisho linakwenda kuwa mapacha, karibu sana kwamba hiyo ingeliwadanganya wateule kama ingewezekana.Unaona?** kanisa linakwenda kuwa….mwendelezo wa Pentekoste inafanana kabisa kama kitu halisi,mpaka ingeliwadanganya yamkini walio wateule.Na baadaye kidigo, kama nikiipata nafasi, Nataka kueleza kile, jinsi ule uteule ulivyokuja unaona.Itaenda kuwadanganya wao,kwa sababu ni kama tu kitu kile kile, mwendelezo ule ule,jambo lile lile, uwanja ule ule mahali ambapo Neno lilianguka bali mmoja wao amepotoka,kwa sababu ni Baba asiye sahihi, nitawathibitishia siku moja ikiwa Mungu ataniruhusu, kwamba madhehebu ni alama ya mnyama.Unaona, ni Baba asiye sahihi.Yeye anawaongoza watu kwenye madhehebu badala ya kwenye Neno la Mungu.Unaona ni Baba asiye

sahihi.Ni mwendelezo wa Kaini.**Nitakapokwenda nyumbani wakati huu, ninahubiri juu ya somo, ''(The trail of the sepent)" ile njia ya nyoka mnyama hapo mwanzo, na mnyama mwishoni,na tunalifuata moja kwa moja kupitia Biblia, na linaonyesha jinsi anavyoenda kuishia.**

Na sasa, **angalia jinsi alivyo mwerevu jamaaa huyu, jinsi alivyo halisi tu katika yake………Kwanini,wao wako kama Yuda na Yesu pale, wote ndugu katika kabila, kama tu Esau na Yakobo. Na kama kunguru na huwa wakiwekwa katika safina ile ile. Na kila kitu ni mapacha katika mfumo ambao tuko ndani yake.Adui anatumia udanganyifu, kama alivyo fanya kwa Hawa, oh, Mungu amesema? Hakika. Hakika…..Unaona? Akijaribu kuhoji nyuma ya kile Mungu alichosema cha asili, ''Mtakufa.Yeye alisema,ndio,Mungu alisema hivyo, bali hakika"….Unaona vile alivyo lipulizia juu yake? Unaona? Bali kile Mungu amesema,Mungu hukitunza; hahitaji msaada wowote kutoka kwa shetani.Yeye hutunza hilo.Hivyo** basi usidanganywe kamwe na kitu hicho.

**Kanisa la kimwili, Kanisa la kiroho.** Kuna kanisa la kimwili ambalo huwa wanawake wanaonyesha kwa mfano,na kuna kanisa la kiroho pia kanisa la kimwili na kanisa la kiroho hawawezi kurithi pamoja.Ni tofauti ni ya nyakati mbili mbali mbali, watu wa tabaka mbili mbali mbali,chini ya agano mbili mbali mbali (Galatia 4:19-31).

Watu wengi waaminifu huenda kujiunga na dhehebu, au kundi fulani, au kikundi kilichojitenga cha namna fulani, na hapo hufa kiroho. Huwezi kuwaambia kitu . Wanashindiliwa takataka hizo, ''Kwa nini maaskofu hawa walisema hili, na huyu alisema hili, huyu alisema hili,na huyu alisema hili,**unawaonyesha papa hapa katika Neno la Mungu ambapo ni BWANA ASEMA HIVI, lakini mchungaji wetu……..''sijali mchungaji wetu anasema nini,sijali msemalo,au mtu mwingine asemalo.Kama ni kinyume cha Neno la Mungu lililo thibitishwa, la saa hiyo wakati huo. Ujumbe ule,na kadhalika Lisahau! Kaa mbali nalo**. Na yanipasa nisimame mbele ya kila mmoja wenu katika siku ya hukumu, nanyi mwajua hilo.Singe thubutu kusema hilo,ni kujua mimi ni mzee sana.Nita……Si kwamba najua kitu, lakini yeye anajua. Nafuata tu yale aliyosema.

Nukuu:
WATIWA MAFUTA WA SIKU ZA MWISHO UK 23 PARA 91,-25 JULAI,1965,
KRISTO AKIFUNULIWA KATIKA NENO LAKE MWENYEWE PARA 27-30
MAMBO YATAKAYO KUWEPO PARA 113-115
NI LAZIMA UZALIWE MARA YA PILI PARA 161-164
ROHO ZINAZO SHAWISHI PARA 89-93
USHAWISHI-14 NOVEMBA-1963; PARA 39-40
ROHO ZINAZO SHAWISHI PARA 152
NENO LILILONENWA NDIO MBEGU YA ASILI UK 5,69-UJUMBE WA KIINGEREZA-PARA 91-92
MAMBO YATAKAYO KUWEPO-PARA114
TUMTENDEJE HUYU YESU AITWAE KRISTO-PARA 130
KUMTENDEA MUNGU KAZI BILA MAPENZI YAKE 65-11-27B; PARA 294-296
UKAMILIFU PARA 35-39
UMOJA PARA 55
KRISTO NI SIRI YA MUNGU ILIYO FUNULIWA UK 87 PARA 572
EDENI YA SHETANI UK 5
NGUVU YA KUBADILISHWA-31 OCTOBER-1965 ASUBUHI:PARA 135-139
MBEGU HAITARITHI PAMOJA NA KAPI –UK 10 PARA 62
KUMTENDEA MUNGU KAZI BILA MAPENZI YAKE18 JULAI 1965 UK 24 PARA 135.



*jiwe la kiroho la kujengea na 115 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebeievers.de*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*